## HALMASHAURI YA WILAYA CHUNYA

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI -TASAF III

Halmashauri ya wilaya ya Chunya ni miongoni mwa Halmashauri zinazotekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii -TASAF III hapa nchini. Mpango ulianza kutekelezwa Mwezi January, 2015 kwa kuzitambua na kuzihakiki kaya za walengwa watakao ingia katika mpango huu katika vijiji vyote vilivyo pata fursa hii. Malipo kwa kaya maskini yalianza Mwezi July, 2015. Jumla ya vijiji **29** katika wilaya yetu vinanufaika na mpango huu na kaya za walengwa **5,527** zinanufaika na mpango huu kwa sasa wa kunusuru kaya maskini.

Mpaka sasa Halmashauri ya wilaya imesha pokea na kutumia kiasi cha **Tsh: 6,228,453,499.45** kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu katika wilaya za Chunya na Songwe. Aidha mpaka sasa walengwa wamesha pokea malipo ya awamu 17 tofauti tangu tuanze kuhawilisha fedha katika wilaya yetu.

### MAFANIKIO YA MPANGO YALIYOPATIKANA MPAKA SASA.

1. Kupungua kwa kiwango cha umaskini kwa kaya za walengwa wanaonufaika na mpango huu. Hii ni kutokana na takwimu mbalimbali tunazozipata na ziara tunazofanya za kuzitembelea kaya hizi za walengwa mara kwa mara.

2. Walengwa wamekuwa na uhakika wa upatikanaji wa chakula na ongezeko la milo katika kaya zao, hii ni kutokana na matumizi sahihi ya fedha za mpango wanazo pata. Kabla ya mpango huu kaya zote 5,527 zilikuwa hazina uhakika kupata milo 3 kwa siku. Kwa sasa takwimu zinaonyesha kuwa kabla ya mpango huu kaya 3,684 sawa na asilimia 66.7% ya kaya zote zilizopo katika mpango zilikuwa zinapata mlo moja tu kwa siku, kaya 1,843 sawa na asilimia 33.3% ya kaya zote ndizo zilikuwa na uwezo kupata milo 2 kwa siku. Kwa sasa kaya zote 5,527 zinapata milo 3 kwa siku. Haya ni mafanikio makubwa sana kwa kaya hizi.

3. Kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi mashuleni na mahudhurio yameboreka sana kutokana na utimizaji wa masharti ya elimu kwa walengwa. Kwa mwaka huu 2018 jumla ya wanafunzi 1,017 wameandikishwa kuanza darasa la kwanza na wanafunzi 137 wamejiunga na kidato cha kwanza katika shule mbalimbali za Sekondari. Tuna jumla ya wanafunzi 5,129 wanaosoma katika shule za msingi 34 na wanafunzi 191 wanaosoma katika shule 7 za Sekondari katika wilaya yetu na maeneo mengine nchini. Takwimu katika fomu za masharti ya elimu zinaonyesha kuwa mahudhurio ya wanafunzi ni kati ya asilimia 95-100% kwa shule zote.

4. Mpango umeongeza juhudi ya wanafunzi kusoma kwa bidii sana kutokana na zawadi zinazotolewa kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo yao kwa kila muhula. Kwa mwaka 2017 jumla ya wanafunzi 71 wanaotoka katika familia za walengwa wa kaya maskini walishika nafasi ya 1, 2 na ya 3 katika mitihani ya mhula wa kwanza na kupatiwa zawadi kama motisha kwao ili kuongeza bidii katika masomo. Katika Mhula wa Desemba 2017 jumla ya wanafunzi 47 wameshika nafasi ya 1, 2, na 3 katika madarasa yao.

5. Vile vile kuwekuwa na ongezeko la matumizi ya kaya katika afya. Katika wilaya yetu jumla ya walengwa 4,994 sawa na 90% ya walengwa wote wamejiunga na Mfuko wa Afya ya jamii (CHF). Katika kuhakikisha kuwa watoto wanahudhuria kliniki bila kukosa kila mhudumu au mganga wa kituo cha afya na Zahanati tumempatia daftari ili kufuatilia kwa karibu afya za watoto wote 2,790 waliopo katika mpango katika wilaya. Tunafurahi kuwajulisha kuwa mahudhurio ya watoto hawa kliniki ni asilimia 98-100% hii ni kutokana na utimizaji wa masharti ya afya na wakimama kuona umuhimu wa kupeleka watoto wao Kliniki.

6. Undwaji wa vikundi vya VICOBA kwa walengwa wa mpango huu, kumekuwa na ongezeko kubwa la walengwa kujiunga katika vikundi vya VICOBA hii ni baada ya kupatiwa elimu toka kwa wawezeshaji wa mpango (PAAF) na maafisa ugani. Katika wilaya yetu mpaka sasa jumla ya kaya 2,020 sawa na asilimia 36.5% ya kaya zote zilizopo katika mpango zimejiunga katika VICOBA. Mpaka sasa tuna jumla ya vikundi 101 vilivyo anzishwa na kusajiliwa kwa baadhi ya vijiji vinavyotekeleza mpango huu. Vikundi hivi vina mtaji wa Tsh: 10,350,000/= Bado tunaendelea kutoa elimu ya VICOBA kwa walengwa ili wajiunge zaidi kwa sababu hii itasaidia kuongeza kipato katika familia zao. Uanzishwaji wa vikundi hivi vya kiuchumi vimewasaidia walengwa hawa kujua taratibu za utunzaji fedha, elimu ya ujasiliamali na faida ya mikopo katika kuongeza kipato.

7. Vile vile tumeweza kushughulikia malalamiko ya walengwa kwa wakati katika vipindi tofauti tofauti mara tulipo yapata. Tulipokea jumla ya malalamiko 107 toka kwa walengwa na kuyashughulikia malalamiko 104 sawa na asilimia 97% ya malalamiko yote tuliyo yapokea. Malalamiko 4 sawa na asilimia 2% yamewasilishwa TASAF makao makuu kwa utekelezaji zaidi.

8. Tumefanya usimamizi na ufuatiliaji katika siku za malipo ya walengwa na shughuli za mpango katika maeneo yote ya wadau tunaoshirikiana nao katika utekelezaji wa mpango huu, maeneo hayo ni shule za msingi 34, shule 7 za sekondari,

Zahanati 18, vituo vya afya 2, vijiji 29 vinavyotekeleza mpango na maafisa ugani 29. Tumefanya ziara moja kwa kila eneo tajwa hapo juu katika kila kipindi cha malipo tangu tumeanza kutekeleza mpango katika wilaya yetu. Katika usimamizi na ufutailiaji huo tulikuwa tunakagua madaftari tuliyowapatia kuandika taarifa zote za mpango na fomu za masharti wanazo jaza.

9. Walengwa kujishughulisha na shughuli za kilimo. Kumekuwa na ongezeko kubwa la walengwa kujishughulisha na kilimo katika kuhakikisha kuwa wanapata chakula cha kutosha ili kuepukana na njaa katika kipindi cha hali. Mpaka sasa jumla ya kaya 3,757 sawa na asilimia 68% ya kaya zote wanajishughulisha na kilimo. Fedha ya mpango imewasaidia kununua mbolea, mbegu ya kisasa na kuweka vibarua ili kuwasaidia katika shughuli za kilimo hivyo kuongeza kipato katika kaya. Walengwa wengi wanalima mazao mchanganyiko ya biashara na chakula kama vile Maharage, Mahindi, Tumbaku, Karanga, Ulezi na Alizeti. Kilimo kimewasaidia walengwa kuwa na uhakika wa chakula katika kaya zao, kujishughulisha na biashara ndogo ndogo na kuwaongezea kipato pia.

10. Mpango umechochea kaya za walengwa kujishughulisha na kazi ambazo sio za kilimo mf, uanzishwaji wa migahawa, viduka vidogo vidogo nk. walengwa wengi kwa sasa wameanzisha miradi midogo midogo kwa ajili ya kuongeza kipato katika familia. Mpaka sasa katika wilaya yetu jumla ya kaya 1,484 sawa na asilimia 27% ya kaya zote zimejiajiri na kuongeza njia nyingine ya kujipatia kipato mbadala ya kutegemea ruzuku ya mpango wanayopatiwa na Serikali.

11. Aidha, Mpango umesaidia sana kuboresha Sera ya kulinda mazingira na kijamii katika vijiji ambavyo vinatekeleza mpango huu katika wilaya yetu ya Chunya. Mpaka sasa jumla ya vijiji 24 sawa na asilimia 82.7% ya vijiji vyote 29 vinavyotekeleza mpango huu vina vyoo, vijiji 12 vina mashimo ya kutupia taka, vijiji 29 vina ulinzi wa kutosha katika siku za malipo ya walengwa, vijiji vyote 29 kuna usafi wa mazingira katika maeneo ya malipo na uwepo wa fursa za makundi maalum(walemavu, wakina mama wajawazito na wanaonyonyesha, wazee, wagonjwa) kuchukua fedha zao mapema katika siku za malipo ya walengwa.

12. Vile vile mpango umesaidia sana kupunguza udumavu wa watoto wanaohudhuria Kliniki toka kwa walengwa. Takwimu zinaonyesha kuwa kabla ya mpango watoto 35 walikuwa katika eneo la rangi nyekundu katika kadi zao za kliniki, watoto 261 eneo la rangi ya kijivu, watoto 1,032 eneo la kijani lakini baada ya kaya hizi kuanza kupata fedha za mpango takwimu zinaonyesha kuwa hakuna mtoto alie katika eneo la rangi nyekundu katika kadi ya kliniki, watoto 113 wapo

katika eneo la rangi ya kijivu na watoto 2,677 wapo katika eneo la rangi ya kijani. Haya ni mafanikio makubwa sana ya mpango katika kuimarisha afya na lishe kwa watoto hawa. Tunaendela kuwaelimisha wazazi wa watoto wa walengwa hawa kuwapatia lishe bora ili watoto wote wawe katika rangi ya kijani katika kadi zao za Kliniki.

13. Walengwa kuboresha makazi, walengwa wengi kwa sasa wameboresha makazi yao na wengine wamejenga makazi mapya ambayo ni bora zaidi ya makazi yao ya awali. Jumla ya kaya 1,161 sawa na asilimia 21% ya walengwa wote wameboresha makazi yao na kaya 574 wamejenga makazi mapya ambayo wamefanikiwa kujenga kwa matofari na kuezeka kwa mabati, haya ni mafanikio makubwa sana kwao.

14. Ufugaji, walengwa wengi wameanzisha shughuli za ufugaji wa mifugo mbalimbali kama vile ufugaji Ng'ombe, Kuku, Mbuzi, Bata, Sungura Nguruwe; kwa ajili ya kujiongezea kipato katika familia. Mpaka sasa jumla ya kaya 1,961 sawa na asilimia 35.4% kati ya kaya 5,527 zimeanzisha ufugaji wa mifugo mbalimbali katika kaya zao. Kaya hizi zina jumla ya mifugo 11,017 ya aina tofauti. Ufugaji huu umewasaidia sana walengwa kujenga na kuboresha makazi yao, kuongeza kipato, kununua mbolea, kununua mavazi na kununua chakula wakati wa hali.

15. Aidha, mpango umeleta ongezeko kubwa la umiliki wa rasilimali kwa kaya za walengwa wa mpango. Takwimu zinaonyesha kuwa walengwa wengi kwa sasa wanamiliki mashamba yao, wamenunua mifugo ya aina mbalimbali (kuku, Nguruwe, Mbuzi, Bata, Ngombe), wamenunua umeme jua na samani mbalimbali za nyumbani.

16. Na la msingi zaidi walengwa wameweza kujiamini, kujitambua na kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo katika vijiji vyao kwa sasa. Kabla ya kuingia katika mpango huu walengwa wengi walikuwa hawajiamini na kujitambua na wengine walikuwa wanaogopa hata kuhudhuria katika mikutano ya hadhara ili kujua maendeleo ya kijiji, mpango huu umewajengea uwezo wa kujiamini na kujitambua kwamba wao pia ni muhimu katika jamii yetu na hivyo wana wajibu wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya vijiji vyao.

## CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO

1. Uhitaji mkubwa wa wananchi katika kutaka kuingia katika mpango huu kutokana na wananchi walio wengi kuwa maskini katika maeneo mengi ya wilaya yetu.

2. Changamoto ya utekelezaji wa mpango huu kwa Halmashauri mbili za Chunya na Songwe kutoka na kila Halmashauri kuwajibika katika mkoa mwingine kiutawala.

3. Ufinyu wa fedha za usimamizi na ufuatiliaji zinazotumwa na TASAF makao makuu hii imepelekea baadhi ya wanakamati ya mpango (CMC) ngazi ya vijiji kuacha kuendelea kusimamia kazi za mpango.

**MIKAKATI YA UTATUZI WA CHANGAMOTO**

- Tumewaandikia TASAF makao makuu barua juu ya taratibu zitakazotumika kwa ajili ya mgawanyo huu kwa Halmashauri ya wilaya za Chunya na Songwe.

- Vilevile tumewajulisha TASAF makao makuu juu ya ufinyu wa fedha za usimamizi na ufauatiliaji.

David Ngowo

Mratibu wa TASAF

**CHUNYA.**